


# JOEL NANAUKA FOUNDATION

## IMPACT REPORT

JANUARY 2024 - JUNE 2024





## 01. Wajane Empowerment Program (WEP)

- Mradi wa mafunzo ya ushonaji na ufumani kwa Wajane umeanza. Mradi huu unalenga kuwapatia ujuzi wa kutengeneza bidhaa ili waweze kujitegemea.
- Tumewasaidia watoto 4 wa wajane kuwarudisha shule kwa kuwalipia ada na kuwapatia vifaa vya shule vinavyohitajika.
- Tumewalipia gharama wajane 5 za usafiri, malazi na chakula kwa Wajane ili waweze kushiriki maadhimisho ya siku ya Wajane kitaifa Morogoro.
- Mchakato wa kukata Bima za Afya kwa wajane 20 umeshaanza. Gharama ya kila mjane ni wastani wa shilingi 200,000/-.
- Kumtafutia makazi na kumlipia mjane mmoja aliyekuwa analala nje ili aweze kupata makazi ya kulala (Amelipiwa kodi ya miezi 3). Tunaendelea kukusanya pesa kwa ajili ya kumlipia kwa mwaka mzima. Mwezi mmoja ni shilingi 100,000/-.

## 02. Wagonjwa waliosaidiwa

Binti anayesumbuliwa na kichwa kikubwa, Vanila amefanikiwa kufanyiwa operesheni tatu MOI (Muhimbili), na sasa ni mwezi wa pili anaendelea kuhudimiwa. Tunatarajia akiwa mzima  kabisa, ataweza kurudi nyumbani mwezi huu.

## 03.Mradi wa ushonaji kwa wasichana wanaotoka kwenye mazingira magumu

- Mradi unawalenga wasichana ambao walilpata ujauzito katika umri mdogo, walioshindwa kuendelea na masomo kutokana na hali mbaya ya kiuchumi n.k
- Jumla ya cherehani 8 zimeshanunuliwa kati ya 20 zilizohitajika.
- Wanafunzi 8 wameanza kupewa mafunzo.
- Mwalimu ameshapewa mkataba na kupewa malipo ya awali.
- Wasichana hawa wanalipiwa gharama zote na taasisi yetu.











# 04.
# Mahitaji ya mavazi na chakula

Mavazi mbalimbali yaliyokusanywa na taasisi yamegawiwa kwa watu wenye mahitaji wakiwemo, watoto, wanawake na wazee katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Kibaha.

Tumepeleka msaada wa chakula kwenye kituo cha watoto wenye uhitaji kwa kushirikiana na Francy Microfinance.

# 05. Program ya afya na lishe kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano (05)

Wanawake 300 na watoto walipewa mafunzo ya vitendo ya namna ya kuandaa lishe bora kwa watoto ili kuepusha utapia mlo na udumavu kwa watoto mkoani Mtwara Kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani.



# 06. Program ya hedhi salama kwa wanafunzi wa shule ya msingi






Wanafunzi 300 wa shule ya msingi walifikiwa kwa ajili ya hedhi salama na kugawiwa pedi.

Tunaomba uendelee kushirikiana nasi:

## LIPA NAMBA

vodacom | m-pesa

**5 4 2 3 4 7 0 0**

JOEL NANAUKA FOUNDATION

## A/C

NMB

**22510098403**

JOEL NANAUKA FOUNDATION

CONTACT:
+255 756 999 996